

Wafanyabiashara mifugo wanolewa kuomba leseni kupitia mitandao

Na Mwandishi Wetu

WAKALA wa Usajili wa Biashara na Leseni (Brela) ipo katika utoaji mafunzo ya siku saba kwa wafanyabiashara wa mifugo waliopo Pugu Mnadani jijini Dar es Salaam, kuhusu upatikaji wa leseni ya biashara kwa njia ya mtandao.

Akizungumzia lengo la mafunzo hayo, Ofisa Biashara wa Brela, Peter Riwa, alisema ni kuwahamasisha wafanyabiashara wa mifugo kurasimisha biashara zao ili wanufaike zaidi.

"Hapa tumelenga kuwafikia wadau wetu na kuwapa elimu juu ya huduma tunazotoa, kuwahamasisha wadau kuhusu umuhimu wa leseni za biashara, kuwasogezea huduma karibu na kutatua changamoto za wadau wetu papo kwa hapo pindi wanapopatiwa elimu hii," alisema.

Alisema hatua hii ni moja ya mkakati wa kuondoa na kupunguza urasimu unaokuzwa na uwepo wa 'vishoka' wanaokwamisha utaratibu katika upatikanaji leseni kwa wafanyabiashara.

Mkuu wa Mnada wa Pugu, Kerambo Samwel, alipongeza hatua ya Brela kuwafikia wafanyabiashara wa mifugo mahali walipo hasa katika eneo hilo la Mnada wa Pugu akisema itawawezesha kupata leseni za biashara kwa urahisi.

Kerambo alisema changamoto wanazokumbana nazo wafanyabiashara wa mifugo ni pamoja na leseni moja ya biashara kutumiwa na zaidi ya mtu mmoja pamoja na kutokuwepo kwa elimu ya kutosha kuhusu upatikanaji wa leseni za biashara.



Na Lucy Lyatuu

Wafugaji zitumieni ranchi, kufuga kisasa na kibiashara

MIGOGORO ya wakulima na wafugaji ni eneo ambalo limekuwa lina changamoto za muda mrefu nchini na mazao mbalimbali ya wakulima yakiharibiwa kutokana na ufugaji usiokuwa wenye tija.

Kutokana na changamoto hizo, wakulima wamekuwa wakiwalalamikia wafugaji, hivyo hivyo na upande huo unaolalamikiwa bila kujali ukiendelea kufuga mifugo yao katika maeneo mbalimbali ikiwamo kwenye mazao ya wakulima jambo lililosabasha maeneo mengine kuwapo kwa matukio ya mapigano.

Katika juhudi za kuhakikisha ufugaji unakuwa wenye tija na uendelevu zaidi, Kampuni ya Ranchi za

Taifa (Narco) hivi karibuni imepangua tozo kwa mikataba mipya ya upangishaji katika vitalu vya uwekezaji vya kampuni hiyo, jambo litakalosaidia uboreshaji wa sekta ya mifugo kwa ujumla.

Sio kwamba kupunguzwa kwa tozo hiyo hadi kufikia Sh 3,500 kwa ekari moja kwa mwaka itasaidia tu kupunguza migogoro ya wakulima na wafugaji, lakini pia ni eneo mojawapo litakazosaidia kufanya sekta ya ufugaji kuwa bora na ya kisasa zaidi.

Aidha, mpango huo utasaidia pia kuwawezesha wafugaji wadogo wanaohitaji kufuga kisasa na kibiashara ili kuondokana na ufugaji wa kienyeji na usiokuwa na tija.

Haina ubishi kuwa bado wapo wafugaji nchini tena wenye mifugo mingi ambao bado wanahama kutoka mkoa mmoja kwenda mwingine kwa ajili ya kutafuta chakula cha mifugo yao, jambo ambalo katika harakati hizo uharibifu wa aina moja hadi nyingine unaweza kutokea.

Inawezekana mlinzi wa mifugo hiyo akapata athari

za kiafya ambazo zinaweza kusababisha kuambukiza katika familia husika lakini pia wanyama wakifugwa kiholela bila kujali lishe bora wanayoweza kuathiri biashara ya mifugo kitaifa na kimataifa kwa ujumla.

Kadhalika ufugaji wa aina hiyo usiokuwa na malengo unaweza kusababisha kuwapo kwa maambukizi ya magonjwa baina ya wanyama au hata kwa binadamu kwa kuwa ni ufugaji wa kuzunguka maeneo mbalimbali.

Hivyo, kwa punguzo la tozo hiyo, wafugaji wanaweza kujiunga katika vikundi na kuunganisha mifugo yao na kupata ardhi katika ranchi, jambo litakalosaidia kuwa na uhakika wa lishe kwa mifugo yao kwa wakati husika na hata kuona fahari ya kufuga kibiashara kwa kutanua soko la ndani na hata la nje.

Ikumbukwe kuwa inaelezwa kuwa Tanzania ni miongoni mwa nchi za Afrika zinazoongoza kwa kuwa na mifugo mingi ambayo kwa namna moja hadi nyingine ikitumika vyema ni

eneo ambalo pia linaongeza pato kwa wafugaji wenyewe na hata kwa taifa kwa ujumla.

Kutokana na kushuka kwa tozo hiyo haitegemewi kuendelea kuwapo kwa makundi ya wanyama ambao bado watakuwa wakizungushwa kutoka mkoa mmoja kwenda mwingine kwa ajili ya kutafuta malisho, la hashani wakati muhimu kwa wafugaji kila mmoja kuanza kutafuta namna ya kuingia mkataba na ranchi ili kufuga kisasa na kibiashara zaidi.

Ikumbukwe kuwa kabla ya tozo hizo kushushwa hapo nyuma kulikuwa na tozo ya Sh 3,000 na 5,000 hadi 7,000 kwa ekari moja kwa mwaka, ambapo wafugaji wakubwa ndio waliokuwa na uwezo wakupata maeneo hayo, lakini kwa sasa kila Mtanzania mwenye nia ya kufuga kisasa na kibiashara anamudu kuchukua eneo hata kwa kuungana.

**MSAMIATI
WA LEO**

Habari 50